

**MAELEZO YA MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO KWENYE  
VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MALIPO YA MADAI YA  
MALIMBIKIZO YA MISHAHARA KWA WATUMISHI  
WA UMMA**

**Ndugu Wawakilishi wa vyombo vya habari,** nimewaiteni leo hii ili niwape taarifa fupi kuhusu malipo ya madai ya malimbikizo ya mishahara kwa Watumimishi wa umma waliokuwa na madai ili muweze kuufikishia umma wa Watanzania.

Serikali kupitia mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara (Human Capital Management Information System – HCMIS) kufikia tarehe 01 Julai 2017 ilikuwa na madai ya malimbikizo ya mishahara yenye jumla ya shilingi 127,605,128,872.81 kwa watumishi 82,111 Wakiwemo walimu 53,925 waliokuwa wanadai shilingi 53,940,514,677.23 sawa na asilimia 42.27 ya madai yote, na wasiokuwa walimu 28,186 waliokuwa wanadai jumla ya shilingi 73,664,614,195.58 sawa na asilimia 57.73 ya madai yote. Madai haya yalikuwa ya muda mrefu mengine yakiwa ya kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2017

Madai haya yalijumuisha mishahara isiyolipwa, tofauti ya mishahara kutokana na kukaimu na nyongeza za mishahara zilizotokana na kupandishwa vyeo na kuchelewa kurekebishiwa mishahara.

**MATOKEO YA UHAKIKI WA MADAI YA SHILINGI BILIONI  
127,605,128,872.81 KWA WATUMISHI 82,111**

- a) Madai ya watumishi 27,389 kati 82,111 yenye jumla ya shilingi **43,393,976,807.23** ikiwa ni asilimia **34** ya madai yote ya shilingi bilioni **127,605,128,872.81** yaliyohakikiwa yameonekana ni sahihi na yanastahili kulipwa bila marekebisho.

b) Madai yanayostahili kulipwa yanajumuisha shilingi bilioni **16.25** kwa walimu **15,919** na shilingi bilioni **27.15** kwa watumishi wasiokuwa walimu **11,470**

**c) Madai yote yaliyoonekana kuwa sahihi ya shilingi bilioni 43.39 yatalipwa pamoja na mshahara wa mwezi Februari 2018 kwa mkupuo mmoja. Malipo ya Madai haya ambayo mengine yana zaidi ya miaka kumi majina ya walipwaji wote yatatangazwa kwenye magazeti kuanzia kesho tarehe 10 Februari, 2018.**

Kwa matokeo hayo ya uhakiki, mazoezi yaliyofanyika likiwemo zoezi la kuwaondoa kwenye Mfumo wa malipo ya mshahara ("payroll") watumishi hewa, vyeti feki na wasio kuwa na sifa na uhakiki wa madai ya malimbikizo ya mishahara uliofanyika limeweza kuokoa jumla ya shilingi bilioni **84.22** ambazo ni sawa na asilimia 66 ya madai yote ya malimbikizo ya awali ya shilingi bilioni **127.61 yaliyokuwa kwenye mfumo ambazo bila zoezi la uhakiki kufanyika zingelipwa wakati zilikuwa hazistahili kulipwa.**

Serikali itaendelea kulipa madai ya watumishi kadiri yanavyojitokeza ili kuondokana na malimbikizo ya aina hii ambayo yanaweza kuisababishia Serikali hasara kwa kulipa madai yasiyostahili.

**Asanteni kwa kunisikiliza**